

# Nishani ya Maua.

Nishani hii ipo katika kundi la viumbe vya asili, huwakilishwa kwa rangi nyeupe



By: Yusuph Mwasiposya

## Utangulizi

- Maua ni nini?

Maua ni mimea iliyo na sehemu zenye mvuto maalumu kwa ajili ya uchavushaji

- Mimea mingi sana ina maua
- Maua mengine ni ya muda mrefu wakati mengine hudumu kwa muda mfupi tu
- Maua mengine huonekana kuwa kama magugu tu, maana mara nyingi huota mahali yasipotakiwa kuota

2

### Tambua aina 45 za maua




### Tambua aina 45 za maua




### Tambua aina 45 za maua




### Baadhi ya sehemu za ua

Pistil au Carpel (sehemu ya kike)



Baadhi ya sehemu za ua

## Stameni (sehemu za kiume)




Baadhi ya sehemu za ua

## Sehemu nyinginezo za ua




Baadhi ya sehemu za ua






- Pistil ni sehemu ya kijani iliyogawanyika kama uma kwa juu
- Stamen ni sehemu yenye rangi nyeupe na vichwa vya njano kwa juu

## Baadhi ya aina za maua

A. Orchid:

- Hili ndilo kundikubwa kuliko yote katika mimea ya maua
- Kuna Zaida ya aina 25,000 za maua katika kundi hili
- Kwa kawaida orchids ni monokotiledoni (mmea wenye mbegu ya ghala moja na usio na mzizi mkuu)
- Muundo wa maua haya umetofautiana kutokana na wingi wa aina zake
- Majani yake yana vena sambamba
- Mfano wa maua haya ni Vanilla, Lady's Slipper, na Orchid

10

## Baadhi ya aina za maua

B. Lily (yungiyungi):

- Mimea mingi ya jamii hii ina vena sambamba
- Mfano wake ni Turk's Cap Lily, kitunguu saumu, kitunguu maji, Trillium, Fawn Lily, Tulip, Hyacinth.

C. Mustard (Haradali)

- Kundi hili zamani liliitwa Cruciferae
- Hii ni kwa sababu limebeba petali zilizopishana
- Mfano wa maua ya kundi hili ni: kabichi, Broccoli, Cauliflower, Brussels sprouts, haradali, Horseradish, Watercress

11

## Baadhi ya aina za maua

D. Cacti

- Cacti ni mmea wa tofauti kuliko mimea yote ya maua
- Hukua vizuri katika maeneo ya jangwa na joto jingi
- Ina muundo wa pekee ambao huusaidia kutunza vema maji
- Utofauti wa majani yake ni miongoni mwa vitu vinavyoifanya cacti kuwa maarufu sana
- Mfano wa maua haya ni: Saguaro, Barrel Cactus, Prickly Pear, masikio ya sungura

12

## Baadhi ya aina za maua

E. Rose (waridi)

- Aina hii ya maua huwa na sepali 5 na petali 5
- Kila ua lina angalau stameni 10
- Maua haya yana hypanthium. Huu ni mfumo kama wa bakuli ambao sepali, petali, na stameni huunganika pamoja kwa chini
- Mfano wa maua haya ni: Rose(waridi), Apple(tufaha), Blackberry, Strawberry, Raspberry, Plum, Peach, Cherry, Pear

13

## Baadhi ya aina za maua

F. Bean (maharagwe)

- Aina hii ya maua huwa na petali 5
- Ovari kuu huiva na kuwa ganda ambalo ndani yake hutokeza mbegu
- Mimea hii kwa jina linguine huitwa legumes
- Upekee wake mkubwa ni kuwa mimea hii hubeba bakteria wengi katika mizizi yake
- Bakteria hawa huchukua hewa ya naitrojeni kutoka katika hewa na kuifannya kutumika na mmea. Kitendo hicho huitwa Nitrogen fixation
- Mfano wa mimea hii ni: Bean(maharagwe), Lupins, Clover(klova), Alfalfa, Peas(njegere), Peanuts(njugu), Soybeans(soya), Lentils(dengu), Mimosa, Kudzu

14

## Baadhi ya aina za maua

G. Parsley (kotimiri)

- Jamii hii ya maua huwa na maua ya pamoja na kuwa kama kishada cha maua
- Maua haya madogo huwa sambamba na petali5, sepali 5 na stameni 5
- Mfano wa maua haya ni: Cumin, Parsley(kotimiri), Carrot (Queen Anne's Lace), Dill, Caraway(kisibiti), Fennel(shamari), Angelica

15

## Baadhi ya aina za maua

H. Bellflower (Maua kengele)

- Maua haya hutoa maziwamaziwa meupe yasiyo na sumu
- Maua haya yana jinsia zote mbili
- Yana muonekano kama wa kengele
- Mara nyingi huwa na maua ya bluu(samawi)
- Hutoa maua yanyotofautiana
- Mfano wa maua haya ni: Bluebell, Harebell, Lobelia, Balloonflower

16

## Maisha ya maua

1. Mbegu huhitaji joto na maji ili ikue
2. Mmea unakua kwenda chini na kwenda juu. Kwenda chini hutoa mizizi ili kusaidia mmea kupata virutubisho na maji, kwenda juu hutokeza majani kisha maua
3. Maua huwa na majani mengi
4. Nyuki na wadudu wengine huvutiwa na maua na kisha husaidia kuchavusha maua
5. Maua yakichavushwa huzalisha mbegu
6. Mbegu zikikomaa zinasambaa kwa njia mbalimbali
7. Kisha mzunguko hijirudia kutoka namba 1

17

## Mimea yenye sumu



upupu

18

## Fanya yafuatayo

Piga picha, au chora maua kisha tengeneza upinde wa mvua kulingana na rangi zake

Mfano:

| Red | Orange | Yellow | Green | Blue | Violet |
|---|---|---|---|---|---|
| ▪ Columbine<br>▪ Rose<br>▪ Tulip<br>▪ Cardinal flower<br>▪ Sweet William | ▪ Daylily<br>▪ Marigold<br>▪ Spotted touch-me-not<br>▪ Butterfly weed | ▪ Goldenrod<br>▪ Daffodil<br>▪ Dandelion<br>▪ Butter-and-eggs<br>▪ Evening Primrose<br>▪ Sunflower | ▪ Maple (tree)<br>▪ Solomon's seal<br>▪ Skunk Cabbage<br>▪ Jack-in-the-pulpit<br>▪ Hellebore | ▪ Bluebell<br>▪ Pansy<br>▪ Lupine<br>▪ Violet<br>▪ Hyacinth<br>▪ Hydrangea | ▪ Clematis<br>▪ Self-heal<br>▪ Tufted Vetch<br>▪ Periwinkle<br>▪ Orchid<br>▪ Lady's slipper |

19

## Fanya yafuatayo

Kabidhi maua yaliyokaushwa yenye sifa zifuatazo: petali 5, petali 4, petali 3, na maua yasiyo na petali

Yafuatayo ni maua pendekezwa kwako

| Five petals | Four petals | Three petals | Apetalous |
|---|---|---|---|
| ▪ Wrinkled rose<br>▪ Wood sorrel<br>▪ Cinquefoil<br>▪ Bladder campion<br>▪ Bouncing bet<br>▪ Chickweed<br>▪ Strawberry<br>▪ Blackberry<br>▪ Nightshade<br>▪ Columbine | ▪ Virginia meadow beauty<br>▪ Bunchberry<br>▪ Lily of the valley<br>▪ Sundrops<br>▪ Common Evening Primrose<br>▪ Cranberry<br>▪ Clematis | ▪ Trillium<br>▪ Arrowhead<br>▪ Dayflower<br>▪ Spiderwort<br>▪ Orchid | ▪ Lamb's quarters<br>▪ White calla lily<br>▪ Hog-peanut |

20

## Fanya yafuatayo

- Tofautisha maumbo ya maua tofauti tofauti, ukiwa umefumbwa macho
- Ni maua gani ambayo umeyaona yaakitembelewa mara kwa mara na nyuki, ndege, vipepeo, na viwavi?
- Litazame ua wakati wa mwanga wa jua kwa dakika 10, na kisha litazame tena wakati wa gizagiza, toa taarifa juu ya utembelewaji wa ua hilo na wadudu. Je ni wadudu gani walitembelea? Je umechunguza ua gani?

21

## Faida za maua

- Hutupatia fedha
- Hutupatia kivuli
- Hutupatia chakula
- Hurutubisha udongo
- Huongeza hewa ya oksijeni katika anga
- Hutumika katika majaribio ya kisayansi
- Hutupatia dawa kwa ajili ya binadamu na Wanyama
- Hutumika kama mapambo
- Huvutia watalii
- Huvutia viumbe wa aina mbalimbali mf: ndege wengi husafiri umbali mrefu ili kufuata aina Fulani ya maua

22

## Hasara za maua

- Hutunza wadudu na Wanyama waharibifu
- Baadhi ya maua huwa na sumu
- Hutoa hewa ya ukaa wakati wa usiku, hivyo si vema kuwa karibu na maua wakati wa usiku
- Huhitaji gharama kubwa katika matunzo

23

## Maua katika biblia

- Zaburi 103:15 – Maisha ya mwanadamu hupita kama maua
- Isaya 35:1 – maua ni ishara ya baraka kutoka mbinguni
- Isaya 40:8 - majani na maua yananyauka, lakini neon la Mungu haliwezi kunyauka wala kubadilika
- Mathayo 6:28 – Yesu alitumia mfano wa maua ili kutuonesha jinsi Mungu anavyotujali

24

## REJEA


- http://en.wikibooks.org/w/index.php?title=Adventist_Youth_Honors_Answer_Book/Nature/Flowers&oldid=2482000
- http://www.realtimerendering.com/flowers/flowers.html


25